KENYA JUNIOR SCHOOLS ASSESSMENT

TIVE ASSESSMENT TEST

KUTATHMINI
1-29-CHI
30-49-KUK
50-79-KUF
80-100-KUZ

GREDI 7

KISWAHILI

JINA: ……
SHULE: ……..
NAMBA YA MTIHANI……TAREHE: …….

INSHA

Kutakuwa na tamasha itakayoshirikisha michezo ya kuigiza, nyimbo n amashairikutoka shule mbalimbali katika kaunti yenu. Andika ratoba ya siku hiyo. (Alama 20)

UFAHAMU **(ALAMA 15)**

Soma taarifa ifuatayo halafu ujibu maswali

Kama kuna jambo ambalo limeiparaganya akili yamahuluki ni kuielewa dhana ya demokrasia. Kiumbe huyu heshi kuuliza mkururo wa maswali. Demokrasia ni nini hasa? Tunaweza kula demokrasia? Ni dude gani hili lina kichwa au mkia pekee yake? Je demokrasia inazuia njaa? Demokrasia ni himaya ya wasomi tu au vilevile ni haki ya mafalahi? Kwa muda mrefu kumekuwa na kinyang'anyiro kikubwa katika jamii ambacho azma na. matokeo yake yamekuwa ya kutatanisha. Baadhi ya watu wamejitokeza kama mchuzi wa ugali na kuzusha zahama ambazo si za kuyumkinika. Vichwa vya adinasi vikafyekwa kwa miundo na maparange na matumbo yakapasuliwa na kuapakaza utumbo na vijusi kila mahali. Shingo zikapigiwa vigingi na kukomewa ardhini. Demokrasia si mchezo wa lelemama. Ni sharti tujifunge vibwebwe tumwage damu na tufe ili tupate demokrasia ya kweli!" Mmoja wa mibabe wa demokrasia alinguruma kadamnasi ya umati huku ngoma za vita zikirindima." Hata Marekani na ulaya walimwaga damu. Mamilioni ya watu walipukutishwa na kimbunga cha demokrasia. Chini walilaliana kama Vimatu na tunutu. Hawa manafiki wanafikiri hatuwajui. Katu hatutakubali